

Twende Pamoja

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



Hutolewa kila baada ya Miezi Sita

Juni -Januari 2013 /2014

Toleo Na 001

Ndani

Halmashauri ya Njombe
yawa ya Tisa Kitaifa
kwenye mbio za mwenge.
Uk.3

Tani 1572 za
vocha kuwanu-
faisha wakulima
wilayani Njombe



Habari
katika picha
Uk.7&8

Madiwani wapitisha bajeti ya Bilioni 22 kwa ajili ya shughuli za Halmashauri mwaka 2014/2015



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw. Paulo S Malala akitoa ufafanuzi wakati wa baraza la madiwani kujadili bajeti ya Halmashauri ya Wilaya mwaka wa fedha 2014/2015

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Njombe wilayani Njombe Mkoani Njombe limepitisha rasimu ya mapendekezo ya bajeti kwa ajili ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Katika mapendekezo hayo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inatarajia kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi 22,998 bilioni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, matumizi mengineyo

na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Akisoma mapendekezo hayo katika kikao maalumu cha kujadili bajeti ya Halmashauri hiyo kilichofanyika katika ukumbi mkubwa wa Halmashauri, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Bw Paulo S Malala, alisema jumla ya shilingi bilioni 10.563 zimeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema Sekta za kipaumbele (Pro poor sectors) katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) ikiwemo Afya, Elimu, Maji, Kilimo na Miundo mbinu, pamoja na Sekta za utekelezaji kwa matokeo makubwa sasa yaani 'Big Results Now' (BRN) ambazo ni Elimu, Maji, Kilimo na Mapato zimetengewa jumla ya shilingi bilioni 7.925 kati ya shilingi

Tahariri

Karibuni wasomaji wetu katika toleo la kwanza la jarida la Twende Pamoja ambalo linatolewa na Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Kuanzishwa kwa jarida hili kunatokana na umuhimu wa wananchi kupata habari ikiwa ni haki ya msingi kwa jamii.

Halmashauri ya wilaya ya Njombe ikiwa inafanya kazi na jamii inawajibu wa kutoa habari kwa wananchi wake juu ya masuala mbalimbali.

Mbali na wajibu huo pia ibara ya 18 (d) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza wazi kuwa kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa kwa

wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Kwa kuzingatia matakwa hayo ya kikatiba Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeamua kuanzisha jarida hili ambalo litakuwa linatoka kila baada ya miezi mitatu.

Ili kutoa fulsa kwa kila mwananchi kuifahamu Halmashauri ya wilaya na shughuli inazofanya Jarida hili litakuwa likitoka kwa njia ya kawaida na pia litapatikana kwa njia ya mtandao (Online) kupitia mtandao wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe ambao ni

www.njombedc.go.tz. Hii itatoa

fulsa hata kwa Mtanzania aliyepo nje ya nchi kuweza kulisoma.

Ni matumaini yetu kuwa jarida litakuwa kiungo kizuri baina ya wananchi na Halmashauri na litaboresha mahusiano. Kupitia jarida hili wananchi wataweza kufahamu shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na Halmashauri pamoja na sera, mikakati na mipango inayofanywa na Jamii na Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Tunawatakia usomaji mwema na tutafurahi kupata maoni na ushauri ili kuweza kuliboresha jarida hili.

Sasa Twende Pamoja!

Linatolewa na Ofisi ya

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya

Njombe.

S.L.P 547 Njombe.

Phone: 026 2782111

Fax: 026 2782857

Email: ded@njombedc.go.tz

info@njombedc.go.tz

njombedc@yahoo.com

Tovuti: www.njombedc.go.tz



1Madiwani waidhinisha Bilioni 22

bilioni 10.563 zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 78 ya bajeti yote ya miradi ya maendeleo.

Bajeti ya Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa mwaka 2014/2015 imeongezeka kwa asilimia 22 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2013/2014 iliyokuwa shilingi 18,772,197,397. Sababu iliyochangia bajeti ya Halmashauri kuongezeka ni ongezeko kubwa la makisio ya miradi ya maendeleo ya Matokeo makubwa sasa hasa katika sekta ya maji.

Bw Malala alivitaja vyanzo vya mapato kuwa ni pamoja na fedha kutoka Serikali kuu, michango ya jamii, wafadhili pamoja na Halmashauri ya Wilaya kupitia mapato ya ndani.

Katika mapendekezo hayo Halmashauri ya wilaya imeweka

maombi maalumu mawili ikiwa ni ombi la shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Njombe katika kijiji cha Matembwe pamoja na shilingi 150,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa gari la Idara ya Elimu Sekondari.

Akizungumzia juu ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji miradi ya maendeleo na shughuli mbalimbali, Malala alisema kuwa kuchelewa kwa fedha za miradi kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ni mojawapo ya changamoto kubwa.

Kuhusu utatuzi wa changamoto hiyo Mkurugenzi huyo alisema kuwa Halmashauri imeandaa mpango wa uwekezaji ili kupata vitega uchumi kwa lengo la kuongeza mapato ya ndani na tayari umetengewa fedha katika bajeti ya 2014/2015. ■

Ijue Halmashauri ya Njombe kiutawala

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni moja kati ya Halmashauri kongwe zinazounda Mkoa wa Njombe. Halmashauri nyingine ni Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Ludewa, Wanging'ombe na Halmashauri za Miji ya Njombe na Makambako.

Halmashauri hii ina eneo la ardhi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 3,134 ambazo ni sawa Hekta 313,400. Awali Halmashauri ya wilaya ya Njombe ilikuwa na Kata 36 lakini kutokana na kugawanywa mara tatu imebakiwa na Kata 11

Mgawanyo wa kwanza ulifanyika mwaka 2007 ambapo ilizaliwa Halmashauri ya Mji wa Njombe na mwaka 2012 Halmashauri hii iligawanywa na kuzaliwa Halmashauri ya Mji Mkambako na mwaka 2013 iligawanywa tena na kuzaliwa Halmashauri ya Wilaya ya Wang'ingombe.

Baada ya mgawanyo huo Halmashauri sasa ina Kata 11, Vijiji 44, Vitongoji 219, vyenye jumla ya Kaya 20,526 huku ikiwa na Jimbo moja la uchaguzi ambalo ni Njombe Kaskazini chini ya mbunge Deo Sanga maarufu kwa jina la "Jah people".

Upande wa viongozi wa kisiasa Halmashauri

ya Wilaya ina Madiwani 14 chini ya Vallence M Kabelege ambaye ndie Mwenyekiti wa Halamshauri ya Wilaya ya Njombe.

Madiwani 11 ni wa kuchaguliwa na viti maalumu wako madiwani watatu wote wanatoka chama cha Mapinduzi (CCM). Kiutendaji Halmashauri hii inaongozwa na Paulo S Malala ambaye ndie Mkurugenzi Mtendaji.

Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, ilionyesha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina watu wapatao 85,747 kati ya hao wanaume ni 40,047 na wanawake 45,700.

Wastani wa asilimia 78 ya wakazi wa Wilaya ya Njombe hujishughulisha na kilimo. Shughuli zingine za kiuchumi ni kilimo cha mboga, matunda na biashara ndogondogo.

Wastani wa pato la mkazi ni shs 753,102/= kwa mwaka kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS, 2011).

Kilimo ni uti wa mgongo wa maendeleo ya wakazi wa Njombe ambapo asilimia 78 ya wakazi wanategemea kilimo kama mhimili wa kuendeshea maisha yao ya kila siku. Mazao ya biashara yanayolimwa ni Chai, Kahawa, Pareto,

Nyanya, Miti na Alizeti. Mazao ya chakula ni pamoja na Mahindi, Viazi mviringo, Ndizi Maharage, Ngano, Viazi vitamu, mhogo, Njegere, Ulezi na Njugu. Mazao mengine ni matunda ikiwa ni pamoja na Nanasi, Parachichi, Matofaa (Apples), Pichezi na

Matunda damu (Plums).

Kwa upande wa sekta ya afya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina kituo cha Afya kimoja ambacho ni kituo cha Lupembe, Zahanati 23 zikiwemo 16 za serikali na zahanati sita ni za watu binafsi na mashirika ya dini.

Halmashauri ya Njombe yaongoza mbio za mwenge mkoa wa Njombe

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mkoani Njombe imefanikiwa kushika nafasi ya kwanza kimkoa katika ukimbizaji wa mbio za mwenge wa uhuru kwa mwaka 2013 ikifuatiwa na Halmashauri ya mji wa Njombe.

Sambamba na ushindi huo Halmashauri ya wilaya imefanikiwa kushika nafasi ya tano kwa Kanda ya Nyanda za juu Kusini huku kitaifa ikishika nafasi ya tisa.

Akitoa taarifa hiyo wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC), Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Sara P Dumba, alisema ushindi huo umetokana na jitihada kubwa zilizofanywa na wadau mbalimbali wa maendeleo katika Halmashauri kwa kuwezesha zoezi la maandalizi kwenda vizuri na kwa kasi

kubwa.

Bi Dumba amewapongeza wadau hao pamoja na kuwataka kuendeleza moyo wa kijitolea na mshikamano katika masuala mbalimbali ili kuweza kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, Bi.Dumba alisema kuwa, miradi yote iliyowekwa mawe ya msingi, kuzinduliwa na kukaguliwa na mwenge wa uhuru ni lazima ikamilike kama alivyoagiza kiongozi wa mbio za mwenge mwaka 2013 Bw. Jumma Ally Simai wakati mwenge ukiwa wilayani Njombe.

amesema kukamilika kwa miradi hiyo kutatokana na uwajibikaji wa viongozi wanaosimamia miradi kwa kushirikiana na jamii nzima kiujumla ili kuendana na mpango wa matokeo makubwa sasa (*Big Results Now*).

Kampeni ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele yaendeshwa.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeendesha kampeni ya umezaji dawa kwa ajili ya magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele zoezi lililo endeshwa katika vituo vyote vya

kutolea huduma za afya.

Katika zoezi hilo la utoaji wa dawa kwa magonjwa ambayo hayapewi kipaumbele ambayo ni usubi, matende, mabusha na kichocho watu 257,797

kati ya walengwa 318,594 wamepewa dawa hizo.

Kampeni hii iliwalenga watu wote wenye umri wa kuanzia miaka mitano na kuendelea bila malipo yoyote.

Halmashauri ya wilaya

ya Njombe ina jumla ya vituo 25 vya kutolea huduma za afya. Kati ya hivyo kituo cha afya kiko kimoja na zahanati 24 huku za Serikali zikiwa 20 zingine ni za watu binafsi na taasisi za dini.

Maduka ya dawa 13 yafungiwa.

Idara ya afya ya Halmashauri ya wilaya ya Njombe imeyafunga maduka ya dawa za binadamu na vipodozi 13 kutokana na kutofuata taratibu.

Kufungiwa kwa maduka hayo kunafuatia zoezi la ukaguzi lililoendeshwa na Idara hiyo ambapo jumla ya maduka ya dawa na vipodozi 70 yalikaguliwa kutoka katika kata 11 zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya Aidha maagizo

yametolewa kwa maduka yaliyofungwa na kuwataka wamiliki wafuate taratibu zilizowekwa ili yaweze kufunguliwa tena.

Idara ya afya imejipanga kuhakikisha inafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maduka ya dawa na vipodozi ili kulinda afya za wananchi pamoja na kuwabaini wale wote wanaovunja sheria na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Maghala ya chakula kukarabatiwa

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeanza kufanyia ukarabati baadhi ya maghala ya mazao ya na kuwataka wananchi kuyatunza na kuyatumia vizuri kuhifadhi mazao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Njombe Bw Paul Malala amesema kwa sasa ukarabati wa maghala 13 unaendelea huku ghala jingine likijengwa.

Amesema ghala

jipya linajengwa katika kijiji cha Ninga chini ya ufadhili wa mradi wa Market Infrastructure Grants (MIVARAF) utakaogharimu kiasi cha shilingi milioni 280 hadi kukamilika kwake..

Ghala la Ninga likikamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua tani 2600 za mazao. K u k a r a b a t i w a kwa maghala haya kutawezesha mazao kutunzwa katika hali ya usalama zaidi.

Mkurugenzi asitisha uvunaji miti usio na Tija kijiji cha Iyembela

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw Paulo S Malala amesitisha uvunwaji wa miti katika msitu wa Iyembela na kuagiza mbao na miti yote iliyovunwa kumilikiwa na Serikali ya Kijiji ili zitumike kwa shughuli za kijiji au kujiongezea mapato.

Usitishwaji wa uvunwaji wa msitu huo unaomilikiwa na Serikali ya kijiji cha Iyembela unafuatia uvunaji

uliokuwa ukiendelea kufanyika kinyume na taratibu kutokana na uongozi wa kijiji kuendelea kuwatambua wanunuzi wa miti walionunua kinyume cha taratibu.

Baada ya kufika katika msitu huo na kujionea uharibifu uliofanywa Bw Malala alisitisha mara moja uvunwaji huo na kuitaka serikali ya kijiji cha Iyembela kuitisha mkutano wa kijiji ili kutengua maamuzi

yasiyokuwa na tija yaliyopitishwa awali kuruhusu kuendelea na uvunaji usiokuwa na tija kwa kijiji hicho.

Malala aliutaka uongozi wa Kijiji kusimamia uondoshaji na uuzaji wa mbao na miti yote iliyopo msituni.



Mkurugenzi Mtendaji akitoa maelezo kwa wavunaji wa miti na mwenyekiti wa kijiji cha Iyembela kuhusu usitishwaji wa uvunaji miti katika msitu wa Iyembela.

Wakuu wa shule waaswa kuweka mikakati ya ujenzi wa maabara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Bw Paulo S Malala amewataka wakuu wa shule za Sekondari wilayani hapa kutumia mbinu mbalimbali ili kufanikisha lengo la Serikali la kila shule kuwa na maabara tatu ifikapo Desemba mwaka 2014.

Akizungumza katika kikao cha pamoja baina ya wakuu wa shule za sekondari zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na baadhi ya wakuu wa Idara Bw Malala aliwataka wakuu hao kushirikiana na watendaji wa Kata na Vijiji katika kubuni na kuweka mikakati ya kufanikisha ujenzi wa

maabara katika shule za sekondari.

Akizungumzia kuhusu makusanyo ya ada na michango mingine ya shule Malala amewataka wakuu hao kushirikiana watendaji wa kata na vijiji na kuweka mikakati ya ukusanyaji wa ada na michango mbalimbali.

“Idara ya elimu sekondari pamoja na fedha kwa maana ya ukusanyaji wa mapato ni moja ya sekta zilizopo katika kutekeleza kwa matokeo makubwa (BRN) hiyo uwekwe mkazo katika kukusanya ada na michango mbalimbali kutimiza lengo la Serikali” alisema Bw Malala.

Wakizungumzia kuhusu changamoto

zinazowakabili katika ukusanyaji wa ada na michango mbalimbali shuleni wakuu wa shule walisema kuwa baadhi ya wazazi kutokuwa na mwamko wa elimu na kuwepo kwa yatima wengi ni changamoto kubwa zinazowakabili.

Waliongeza kuwa kitendo cha kuwarudisha wanafunzi nyumbani baadhi ya wazazi hufurahia na kuichukulia kama fulsa ya mtoto kuacha shule. Waliongeza kuwa kuna baadhi ya wazazi huwa hawatoi michango shuleni kwa kisingizio kuwa walisomba tofali.

Kwa upande wake afisa Elimu ya Sekondari Bw Isaack Mgaya amewataka walimu

wakuu hao kusimamia taaluma na kuhakikisha walimu wanafundisha na wanafunzi wanasoma. Bw. Mgaya aliwaagiza walimu hao kuhakikisha kuwa shule zenye hosteli wanafunzi wanakaa katika hosteli.

Sambamba na hilo aliwataka kuhakikisha kuwa bodi za shule zinakuwa hai na kufanya vikao vyao kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Halmashauri ya wilaya ya Njombe ina shule za Sekondari 12 ambapo shule za serikali zipo 10 na shule zinazomilikiwa na watu inafsi ziko mbili. Katika shule 12 zilizoko katika Halmashauri ya wilaya shule mbili tu zilizo na kidato cha tano na sita

Zaidi ya miti milioni 22 yapandwa wilayani Njombe.

Wilaya ya Njombe inatarajia kuotesha na kupanda miche ya miti aina mbalimbali zaidi ya 22,885,650. Kufuatia kuoteshwa na kupandwa kwa miti hiyo wilaya imefanikiwa kuvuka lengo iliyokuwa imejiwekea ambalo lilikuwa ni kupanda miche 15,000,000 kwa mwaka 2013/2014.

Katika idadi hiyo Halmashauri ya wilaya ya Njombe inatarajia kuotesha na kupanda miche ya miti 8,435,466 huku Halmashauri ya Mji Njombe ikipanda miche 14,450,184.

Katika kutekeleza kampeni ya upandaji wa miti wilayani Njombe

maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na hifadhi ya vyanzo vya maji, maeneo yaliyo wazi, maeneo ya mashamba ya mazao kwa dhumuni la kuongeza na kuboresha rutuba na hifadhi ya ardhi, mashamba kwa ajili ya kupata mbao, kuni, fito mkaa na kurekebisha mabadiliko ya tabia nchi.

Uzinduzi wa upandaji miti mwaka 2014 kwa Wilaya ya Njombe umekwenda sambamba na kauli mbiu isemayo “Miti ni mali, panda miti kwanza ndipo ukate” ambapo mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa wilaya ya Njombe Bi Sara Dumba ambaye aliwakilishwa na makamu

mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw. Shaibu Masasi.

Katika siku ya uzinduzi jumla ya miti rafiki ya maji aina ya miwengi 360 ilipandwa katika chanzo cha maji Lupembe barazani kwa ajili ya kuhifadhi na kuboresha chanzo hiki cha maji ambacho kinatumiwa na wakazi wa Lupembe pamoja na kiwanda cha chai Ikanga.

Aidha katika mpango wa hifadhi ya mazingira unaoratibiwa na kiwanda cha chai Ikanga jumla ya miche 800 rafiki wa maji aina ya mivengi imepandwa katika vyanzo mbalimbali vya maji katika tarafa ya Lupembe.

Watendaji wa Kata watakiwa kuwasimamia watendaji wa Vijiji

Watendaji wa Kata za Halmashauri ya wilaya ya Njombe wametakiwa kuwasimamia kikamilifu watendaji wa vijiji katika ukusanyaji wa mapato.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa baraza la madiwani wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Vallence M Kabelege alisema kuwa baadhi ya watendaji wa vijiji wamekuwa hawawajibiki ipasanyo katika ukusanyaji wa mapato.

Aliwataka watendaji wa Kata kuwasimamia kwa ukaribu Watendaji wa Vijiji ili kuweza kudhibiti upotevu wa mapato na kuongeza kuwa Halmashauri haiwezi kuendelea kuvumilia wazembe wachache wanaokwamisha maendeleo.

“Baadhi ya watendaji wa vijiji wamekuwa hawawajibiki ipasavyo katika ukusanyaji wa mapato, badala ya kukusanya wao wamekuwa wakiwateua watu ambao sio waaminifu jambo linalochangia kushuka kwa mapato, naomba muwafikishie salamu zangu.”

Alisema Kabelege.

Alibainisha maeneo ambayo watendaji wa vijiji wanayafanyia uzembe ni pamoja na minada, magulio na mageti ambapo wamekuwa na kawaida ya kuwaachia watu wengine ambao sio waaminifu kufanya kazi ya kukusanya mapato.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe, Bw Paulo S Malala kuwatupia jicho la karibu watendaji hao ili kuimarisha na kufikia lengo la Halmashauri la kukusanya kiasi cha shilingi 496, 649,846 ambayo

ni mapato ya ndani pekee.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 Halmashauri ya wilaya ya Njombe imekadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 32.104 kutoka katika vianzia vyake mbalimbali vya mapato.

Toka vyanzo vya ndani Halmashauri ya wilaya imekadiria kukusanya jumla ya shilingi 637,524,559. Ruzuku ya mishahara na matumizi ya kawaida kwa Idara za Ruzuku inakadiriwa kupokea bilioni 25.673 na ruzuku ya miradi ya maendeleo inakadiriwa bilioni 5.793.



Baadhi ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakiwa katika mkutano wa baraza la madiwani ukumbi wa Halmashauri

Tani 1572 za vocha kuwanufaisha wakulima wilayani Njombe.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa mwaka 2013/2014 imepokea vocha 29,475 sawa na tani 1572 zenye jumla ya Tsh 884,250,000 kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo wilayani hapa.

Vocha zilizopokelewa ni pamoja na mbolea ya kupandia (minjingu mazao) mbegu bora (chotara) pamoja na mbolea ya kukuzia.

Upande wa mbolea ya kupandia (minjingu mazao) jumla ya vocha 9,825 ambazo ni sawa na tani 982.5 zenye thamani ya shilingi

393,000,000 zimepokelewa. Upande wa mbegu bora (chotara) vocha 9825 ambazo ni sawa na tani 8.25 zenye jumla ya thamani ya shilingi 196,500,000 milioni zimepokelewa.

Vocha zote zilizotakiwa kuletwa Halmashauri ya Wilaya na serikali kuu zimeletwa na kupokelewa katika awamu mbili.

Awamu ya kwanza vocha 5000 za mbolea ya kupandia na vocha 5000 za mbegu bora za mahindi zilipokelewa na kugawanywa katika kata za Ikuna, Ninga, Kideg

embye, Matembwe, Lupembe, Ikondo, Idamba na Mfriga kulingana na mgao uliopitishwa na kamati ya vocha ya Wilaya.

Awamu ya pili zimepokelewa vocha 4825 za mbolea ya kupandia na vocha 4825 za mbegu bora za mahindi. Tayari vocha hizi zimeshagawiwa katika kata za Mtwango, Igongolo, Kichiwa kulingana na mgao wao. Katika awamu hiyo ya pili zilipokelewa vocha 9825 za mbolea ya kukuzia na zimegawiwa katika kata zote 11 kwa kufuata mgao uliopitishwa.



Waziri mkuu Mizengo Pinda akipata maelezo ya kilimo hai cha nanasi katika kijiji cha Madeke wilayani Njombe alipofanya ziara kijijini hapo.



Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakiwa katika kikao cha baraza la ushauri la wilaya ya Njombe (DCC)



Wajumbe wa baraza la ushauri la Wilaya ya Njombe (DCC) wakifuatilia rasimu ya bajeti ya Halmashauri ya wilaya ya Njombe ya mwaka 2014/2014.



Wajumbe wa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wakiwa na wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya wakikagua chanzo cha maji kijiji cha Image



Kaimu afisa Maliasili Paulo Libenanga aliyenyosha mkono akitoa elimu juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji wakati wa uzinduzi wa upandaji miti kiwilaya katika Tarafa ya Lupembe kwenye chanzo cha maji Barazani



Wananichi wakishirikiana na wataalamu kupanda miti rafiki ya maji katika chanzo cha maji barazani Lupembe siku ya uzinduzi wa upandaji miti wilaya ya Njombe.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (wa pili kushoto) akiangalia uharibifu uliofanywa katika msitu wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe uliopo kijiji cha Iyembele Kata ya Matembwe.



Wataalamu wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe wakiwa katika kikao cha baraza la madiwani kilichojadili utekelezaji wa shughuli robo ya pili.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe akitoa maelekezo kwa mwenyekiti wa kijiji cha Iyembela kuhusu kusitishwa kwa shughuli zote zinazofanywa katika msitu wa Iyembela.



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw Paulo Malala akikagua ujenzi wa maabara katika shule ya sekondari Lupembe



Wafanyakazi waliokuwa wakipasua mbao katika msitu wa Afisa manunuzi wa Halmashauri ya wilaya ya Iyembela ambao mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya Njombe Bw Martia Nkomola akitoa maelezo alisitisha upasaaji huyo. Mwenye suti ni afisa Elimu (S) Isaack wakati wa utiaji saina wa mikataba na Mgaya akisisitiza jambo.

